JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA KAZI NA MAENDELEO YA VIJANA**

# SERA YA TAIFA YA MAENDELEO YA VIJANA



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# SERA YA TAIFA
# YA MAENDELEO YA VIJANA

**WIZARA YA KAZI NA MAENDELEO YA VIJANA**

**1996**

# DIBAJI

Hili ni toleo la kwanza la Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana. Umuhimu wa Sera ya Vijana ni mkubwa hasa katika kipindi hiki ambacho vijana, wazazi, walimu na jamii nzima kwa ujumla tunaishi na kuendesha harakati mbalimbali katika ulimwengu unaobadilisha teknolojia, mitindo, itikadi, tamaduni na mitazamo haraka haraka. Tanzania pia imekumbwa na mabadiliko hayo ambayo athari zake ni pamoja na hali ya uchumi kushuka; kufifia kwa taratibu nzuri zilizowekwa na jamii za kuwalea vijana; kupotea kwa maadili mazuri miongoni mwa jamii pamoja na kushuka kwa heshima ya mwanadamu.

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana inatoa mwongozo si tu kwa vijana, wazazi na waelimishaji bali kwa jamii nzima na hasa kwa wapangaji wa mipango ya maendeleo katika sekta mbalimbali za maendeleo.

Wizara inatarajia kwamba sera hii itakuwa chombo muhimu kitakachowezesha sekta zinazohusika na maendeleo ya vijana kubuni mikakati na mipango kwa ajili ya vijana, mipango ambayo itawawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za ujenzi wa uchumi na hivyo kuinua pato la Taifa.

**Mhe. S. R. Kinyondo (MB)**
**WAZIRI WA KAZI NA MAENDELEO YA VIJANA**

## YALIYOMO

**Dibaji** .................................................. iii
**Shukrani** .................................................. iv
**Utangulizi** .................................................. ix

**SURA YA KWANZA**

**1.0 HALI HALISI YA VIJANA ILIVYO TANZANIA** .................................................. 1

1.1 Maana ya Kijana .................................. 1
1.2 Idadi ya Vijana .................................. 1
1.3 Hali ya Vijana Kiuchumi ........................ 2
1.4 Hali ya Vijana Kisiasa ........................... 3
1.5 Hali ya Vijana Kijamii ........................... 4
1.6 Hali ya Elimu na Mafunzo ya Vijana ....... 6
1.7 Haki za Vijana .................................. 7

**SURA YA PILI**

**2.0 UMUHIMU WA SERA YA MAENDELEO ......** 9

**SURA YA TATU**

**3.0 MADHUMUNI YA SERA YA MAENDELEO YA VIJANA** .................... 11

**SURA YA NNE**

**4.0 MALENGO NA MIPANGO YA MAENDELEO YA VIJANA** .................... 12

4.1 Malengo ............................................ 12

4.2 Mipango ............................................ 13

## SURA YA TANO

5.0 MAJUKUMU YA SEKTA MBALIMBALI KATIKA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO YA VIJANA ........................ 14

5.1 Familia ........................................................ 15
5.2 Serikali za Vijiji .......................................... 16
5.3 Ardhi, Nyumba na Maendeleo Mijini .......... 16
5.4 Afya ........................................................... 17
5.5 Biashara na Viwanda .................................. 17
5.6 Elimu .......................................................... 18
5.7 Fedha .......................................................... 18
5.8 Kilimo ......................................................... 19
5.9 Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto .................... 19
5.10 Maliasili na Utalii ....................................... 20
5.11 Madini na Nishati ...................................... 20
5.12 Habari na Utangazaji .................................. 20
5.13 Sheria na Katiba ......................................... 20
5.14 Tume ya Mipango ....................................... 21
5.15 Serikali za Mitaa ........................................ 21
5.16 Mashirika yasiyo ya Serikali na Makampuni Binafsi ................................... 21
5.17 Baraza na Kamati za Maendeleo ya Vijana .. 21
5.18 Muundo wa Baraza ..................................... 23
5.19 Wajibu wa Kamati za Maendeleo ya

**TAMATI** .................................................................... 25

KIAMBATISHO NO. 1 .................................................... 27
KIAMBATISHO NO. 2 .................................................... 31

# SHUKURANI

Idara ya Maendeleo ya Vijana inapenda kuwashukuru kwa dhati watu binafsi na mashirika ambayo yalichangia kwa njia moja au nyingine kukamilisha sera hii.

Tunathamini michango yao waliyotoa katika kukamilisha sera hii. Shukrani zetu za dhati ziwaendee wote walioshiriki ambao, kutokana na tatizo la nafasi hatuwezi kuwataja mmoja mmoja.

Hata hivyo tungependa kuwataja wafuatao kutokana na mchango wao muhimu. Hawa ni Bibi Deborah Nyakirangani wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto, Dk. Yohana Mashalla wa Shirika la Afya Muhimbili, Dk. S. Tungaraza wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Bwana Ulinyalusya Tenende wa Tume ya Mipango - Kitengo cha Idadi ya Watu. Bwana Emmanuel Mollel wa Idara ya Sanaa na Lugha, Bi Vivian Nankurlu, Bibi Esther Mwakalasi na Bibi Venerose Mtenga, wote kutoka Idara ya Maendeleo ya Vijana, kwa juhudi zao katika kuratibu shughuli za ukamilishaji wa sera hii.

Na mwisho tunatoa shukurani zetu za dhati kwa mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA) hapa nchini Bwana J. Bill Musoke pamoja na Shirika lake kwa kuwezesha kuchapa sera hii.

Walter M.S. Mazzuki
MKURUGENZI WA MAENDELEO YA VIJANA

## UTANGULIZI

### Usuli

Tangu Tanzania ipate Uhuru wake mnamo mwaka 1961 hapakuwa na Sera rasmi iliyoandaliwa kwa ajili ya malezi na maendeleo ya Vijana. Masuala ya malezi na maendeleo ya vijana kwa kipindi chote hicho yalikuwa yakitekelezwa kupitia Sera nyingine katika mipango ya maendeleo, kampeni, maazimio na miongozo mbalimbali ya Chama Tawala na Serikali.

### Uhalali wa Sera

Msingi wa Sera hii unatokana na uzingatiaji wa haki za binadamu kama zilivyotajwa katika katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kufanyiwa marekebisho mwaka 1984 na 1995. Haki hizi ni pamoja na haki ya kuishi, kulindwa, kuendelezwa na kujiendeleza, kushirikishwa katika shughuli za maendeleo yake na ya jamii. Haki nyingine kulingana na katiba hiyo ni pamoja na haki ya kutobaguliwa, kuheshimiwa, kumiliki mali na rasilimali, kufanya kazi na kupokea matunda ya kazi hiyo pamoja na haki mbele ya sheria za nchi.

Kwa ujumla Tanzania inasisitiza kuwa na jamii ambayo kila raia anahakikishiwa usawa, haki mbele ya sheria, uhuru na nafasi ya kushiriki na kutumia uwezo na vipaji vyake katika shughuli za maendeleo ya jamii, uongozi, utamaduni, uzalishaji mali pamoja na kunufaika na huduma za jamii zilizopo katika kuendeleza na kuboresha maisha yake.

## SURA YA KWANZA

## 1.0 HALI HALISI YA VIJANA ILIVYO TANZANIA

### 1.1 Maana ya Kijana

Maana ya kijana inaweza kutofautiana kulingana na mila, desturi, na tofauti za maadili katika jamii mbalimbali na mahali walipo. Kijana ni mvulana au msichana ambaye yumo katika rika la utoto kuelekea rika la utu uzima. Kutokana na tofauti hizo, sera hii imetumia tafsiri ya kijana kufuatana na tamko la Umoja wa Mataifa ambalo kijana ni mtu mwenye umri kuanzia miaka 15 hadi 24. Katika umri huu jamii inamtazamia kijana aanze kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo na pia aanze kujitegemea kwa kiasi fulani. Kijana anakuwa amebalehe na kuanza kukomaa kifikra. Kutokana na hali hiyo, huanza kuonyesha msimamo kuhusu mambo mbalimbali. Kijana ni mtu anayeonyesha ujasiri katika kufanya maamuzi na matendo yake lakini pia ni katika kipindi hiki baadhi ya vijana huanza kuonyesha woga katika kudiriki na kufanya maamuzi.

### 1.2 Idadi ya Vijana

Kulingana na makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 1995 idadi ya vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 ilikuwa 5,617,100 ambayo ni asilimia 20.6 ya idadi ya watu wote Tanzania (27,323,600). Kati ya vijana hao wavulana walikuwa 2,770,600 (asilimia 49.3) na wasichana walikuwa 2,846,500 (asilimia 50.7). Vijana wengi wanaishi

vijijini ingawa kuna hali ya kuhama vijijini na kuhamia mijini.

## 1.3 Hali ya Vijana Kiuchumi

Shughuli za vijana zinategemea mahali vijana walipo kijiografia, umri wao, jinsia, na rasilimali zilizopo. Hata hivyo, kwa jumla vijana hapa Tanzania wanafanya shughuli zifuatazo:-

1.3.1 Baadhi yao ni wazalishaji mali katika sekta za kilimo, uvuvi, uchimbaji madini, ufugaji na katika viwanda vidogo vidogo kwa mfano useremala, ushonaji, uhunzi n.k.

1.3.2 Vijana wengine hujishughulisha na biashara ndogo ndogo kama vile uuzaji wa nguo, matunda na vyakula mbalimbali. Ingawa baadhi ya vijana wamejiajiri katika sekta ya uzalishaji na biashara, vijana hawa wanakabiliwa na matatizo ya uendeshaji wa shughuli zao. Baadhi ya matatizo hayo ni pamoja na ukosefu wa mitaji, nyenzo, utaalamu au ujuzi n.k.

1.3.3 Kuna idadi ndogo sana ya vijana (asilimia 3.4) ambao wanafanya kazi za kuajiriwa serikalini na katika taasisi za umma na mashirika ya watu binafsi. Kundi hili ni sehemu ndogo tu ya vijana wote waliosoma na kupata ujuzi katika taaluma na fani mbalimbali. Hata hivyo kutokana na sera ya urekebishaji uchumi, vijana wengi waliosoma wameachishwa kazi na wengi wao hawategemei kupata ajira kabisa katika sekta rasmi. Tatizo la

ukosefu wa ajira ni la vijana wote (wasichana na wavulana), lakini wasichana ndio wameathirika zaidi kwa kuwa wengi wao hufanya shughuli zenye ujira mdogo na zisizo za kiufundi.

1.3.4 Vijana walio wengi, asilimia 60 ya wale wote wasio na ajira rasmi nchini hawana kazi maalum. Matokeo yake baadhi yao hujiingiza katika vitendo viovu kama vile wizi, ujambazi, uvutaji bangi, uzururaji, utumiaji madawa ya kulevya, umalaya n.k. Aidha baadhi ya vijana wameendelea kuwa tegemezi kwa wazazi wao hasa katika maeneo ya mijini.

## 1.4 Hali ya Vijana Kisiasa

Kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa chini ya mfumo wa chama kimoja cha siasa. Vijana wamefanya kazi za chama za uhamasishaji umma kama vile vijana wa chipukizi. Vile vile vijana wengi walishiriki katika maamuzi mbalimbali ya kisiasa. Aidha vijana waliandaliwa kushika nafasi za uongozi kupitia jumuia ya chama chao. Katika kipindi cha mfumo wa vyama vingi vya siasa, vile vile vijana wameendelea na dhima hiyo pamoja na shughuli mbalimbali za vyama vyao. Hata hivyo wasichana wachache tu hujitokeza katika uongozi na uwakilishi katika kutoa maamuzi. Kulingana na katiba ya nchi kila kijana mwanamke au mwanaume mwenye umri usiopungua miaka 18 anayo haki ya kupiga kura kumchagua kiongozi anayempenda pamoja na kugombea uongozi katika ngazi mbalimbali.

## 1.5 Hali ya Vijana Kijamii

1.5.1 Kutokana na udhaifu wa utamaduni wa mwafrika, na mabadiliko ya mfumo wa maisha katika jamii yetu ikichangiwa na hali ngumu ya uchumi, utaratibu wa malezi umesambaratika. Hii imepelekea suala la malezi ya watoto na vijana kuwa la waalimu na taasisi nyingine zinazoshughulikia vijana. Aidha suala la malezi katika ngazi ya kaya limeachwa kuwa jukumu la kinamama na kwa kuwa wanawake ndio wenye jukumu kubwa la kutunza familia, muda wao mwingi wanatumia katika kutafuta mahitaji hivyo hubaki na muda mchache sana wa kuweza kutoa malezi yanayostahili kwa vijana. Ugomvi na mifarakano katika ndoa nyingi imesababisha ukosefu wa amani na utulivu katika familia na hivyo kuathiri malezi ya vijana.

Mabadiliko ya maadili ya malezi, kama ilivyo katika matatizo yanayotokana na uchumi, yanapelekea vijana kuvunja sheria na kujiingiza katika vitendo viovu. Vijana wengine hukimbia nyumbani kwao na kujiingiza katika tabia za uzururaji mitaani na uvunjaji wa sheria za nchi. Na wengine hupata mimba katika umri mdogo na kuhatarisha maisha yao katika kujaribu kutoa mimba au kuzaa katika umri mdogo.

Aidha baadhi ya tamaduni za kigeni, kupitia vyombo vya habari na technolojia za kisasa zimeathiri mfumo wa utamaduni wa jamii za Kitanzania. Upungufu huu umesababisha vijana

wengi kuchanganyikiwa, kupoteza na kukosa msimamo katika maisha. Kutokana na tatizo hilo kuna haja ya kuweko na matumizi mazuri ya vyombo vya habari ili kuimarisha utamaduni sahihi na malezi mazuri kwa lengo la kuendeleza vipaji vyao.

1.5.2 Kwa ujumla kundi la vijana ni kundi la watu wanaoonekana na kufikiriwa kuwa na afya nzuri ikilinganishwa na makundi mengine, jambo ambalo limesababisha Serikali kutokuwa na mipango maalumu ya kuwahudumia vijana kiafya. Lakini hali halisi inaonyesha kuwa vijana wanayo matatizo mengi ya kiafya ingawa athari za baadhi ya matatizo haya haziwezi kuonekana mara moja.

Matatizo haya ni pamoja na:-

1.5.2.1 Kuongezeka kwa magonjwa ya zinaa na ukimwi (STD, HIV/AIDS).

1.5.2.2 Lishe duni inayosababisha kudumaa, upungufu wa damu na kuzaliwa watoto wenye uzito mdogo n.k.

1.5.2.3 Utumiaji wa madawa ya kulevya ambayo husababisha magonjwa ya akili na kuwafanya vijana kujiingiza katika vitendo viovu.

1.5.2.4 Tohara kwa wasichana.

1.5.2.5 Kuolewa na kuzaa katika umri mdogo.

Aidha kuna upungufu mkubwa sana wa huduma zinazolenga kuwasaidia vijana kukidhi mahitaji yao kiafya.

## 6 Hali ya Elimu na Mafunzo ya Vijana

Takwimu za Wizara inayoshughulikia elimu zinaonyesha kuwa vijana wanaohitimu elimu ya msingi hawapungui 400,000 kila mwaka. Kati ya vijana hao ni asilimia 10 tu ambao hupata nafasi ya kuendelea na elimu ya Sekondari katika shule za Serikali na zisizo za Serikali. Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa vijana 20,000 tu humaliza elimu ya Sekondari kila mwaka hapa nchini. Aidha, vijana wanaopata nafasi ya kuingia katika vyuo mbalimbali na vyuo vikuu inakadiriwa kuwa ni 10,000 tu kwa mwaka.

Idadi ya wanafunzi wavulana na wasichana walioko katika shule za msingi haitofautiani sana. Kulingana na takwimu za Wizara inayoshughulikia elimu nchini, kati ya mwaka 1982 hadi 1990 wasichana walikuwa asilimia 49 na wavulana asilimia 51 ambapo katika shule za sekondari wasichana walikuwa asilimia 33 tu ukilinganisha na asilimia 67 ya wavulana. Hata hivyo wasichana wengi hasa wa shule za Msingi huathiriwa na tatizo la kupata mimba kabla ya kumaliza masomo yao. Kwa mfano kati ya mwaka 1982 na 1986, jumla ya wasichana 22,133 walikatisha masomo yao katika shule za msingi kwa sababu ya kupata mimba. Pia wasichana wengi hupendelea masomo ya sayansi ya jamii ukilinganisha na wavulana ambao wengi wao hupendelea masomo ya sayansi. Hali hii huathiri wasichana katika uchaguzi wa kazi.

ılio wengi Tanzania wamemaliza elimu ya msingi. yanayotokana na uduni wa elimu yanawaathiri a njia zifuatazo:-

ijana wanaomaliza elimu ya msingi wanakuwa ıtika umri mdogo kuweza kujitegemea na pia anakuwa hawana stadi za kuwawezesha kujiajiri.

adi ya wasichana huendelea kushuka kadri ya adarasa yanavyoendelea. Hali hii huathiri aendeleo yao katika ajira na hata katika kupata adaraka ya uongozi.

toro wa wanafunzi shuleni kutokana na mazingira ıni ya elimu ambayo hayatoi hamasa kwa vijana ıendelea na masomo. Kwa mfano ukosefu wa re za shule, ukosefu wa chakula cha kutosha uleni, ukosefu wa vifaa, madawati , idadi kubwa ı vijana katika darasa moja, vifo n.k.

**'ijana**

vijana kama raia wengine zimewekwa bayana tiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. ı haki zinazowagusa vijana moja kwa moja ni atazo:-

ıki ya kila mtu kujielimisha katika fani ayoipenda hadi kufikia upeo wa juu kulingana na vezo wake. Hali halisi ya vijana kielimu ni vamba kutokana na uhaba wa nafasi za ıjiendeleza vijana wengi wameshindwa

kujielimisha katika fani wazipendazo, aidha wameshindwa kufikia upeo wautakao.

1.7.2 Haki ya usawa. Watu wote, wakiwemo vijana ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote kulindwa. Kutokana na udhaifu wa vyombo vya sheria katika kutekeleza sheria, baadhi ya vijana hasa mijini wamekuwa wakiadhibiwa kwa njia ya kuchomwa moto au kupigwa hadi kufa na raia wengine kwa tuhuma za wizi kabla ya kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria ili kuthibitisha kuwa wanayo hatia ya kutenda makosa hayo. Aidha vijana wa kike katika baadhi ya mikoa wamekuwa wakiteswa au kupata maumivu makali kutokana na mila potofu k.m. tohara za kike.

1.7.3 Haki ya kuishi mahali popote. Japokuwa katiba ya nchi inasema bayana kuhusu haki ya kuishi mahali popote katika Jamhuri na uhuru wa mtu kwenda atakako, lakini ukosefu wa ajira kwa vijana umefanya vijana wajiingize kwenye vitendo viovu na hivyo kufanya vyombo vya dola kuwarudisha makwao. Pia kutokana na hali ngumu ya maisha, vijana wengi siku hizi wameshindwa kupata hifadhi ya maisha yao na huduma muhimu kama vile lishe, malazi, nguo na afya kutoka kwa wazazi. Hali hii imepelekea vijana kutoka sehemu moja na kuhamia sehemu nyingine wakitafuta maisha.

1.7.4 Haki ya kufanya kazi na kupata ujira wa haki. Pamoja na kuwa kuna haki ya kufanya kazi, vijana wengi siku hizi wanaomaliza masomo yao katika ngazi mbalimbali hawapewi haki hiyo katika sekta

rasmi kwa sababu ya hali mbaya ya uchumi. Pia kufanya kazi kwenye sekta isiyo rasmi imekuwa ni vigumu kutokana na mazingira magumu ya kupata mitaji, nyenzo za kufanyia kazi na mahali pa kufanyia kazi zao.

Aidha, licha ya baadhi ya vijana kufanya kazi zaidi ya masaa 8 kwa siku hususan wafanyakazi wa nyumbani, viwandani na biashara za watu binafsi kama vile mabaa, wamekuwa wakipata ujira mdogo ukilinganisha na masaa ya kazi, hivyo kuathiri haki yao ya kupata ujira wa haki.

1.7.5 Haki ya faragha na usalama kwa vijana pia imeathirika vibaya. Vijana, hasa wafanyakazi wa nyumbani wamekuwa wakinyanyaswa na kudhalilishwa kijinsia, na hivyo kuathiri haki ya mtu kupata faragha, kuheshimiwa na usalama wake.

# SURA YA PILI

## 2.0 UMUHIMU WA SERA YA MAENDELEO YA VIJANA

Kutokana na nguvukazi kubwa waliyonayo, vijana ni kundi la watu lenye nafasi na umuhimu wa pekee katika maendeleo ya ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla. Vijana katika jamii ndio wanaopaswa kujihusisha na shughuli nyingi za uzalishaji mali, ulinzi na usalama, utamaduni pamoja na utoaji wa huduma mbalimbali. Aidha vijana wake kwa waume, ndio wenye nafasi nzuri na uwezo mkubwa wa kuendelezwa na kupatiwa maarifa na ujuzi

ikiwa ni pamoja na kushirikishwa katika utoaji wa maamuzi mbalimbali.

2.1 Utaratibu wa kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi ni ule wa kuwashirikisha watu wote wenye uwezo wa kufanya kazi katika kupanga, kuamua na kutekeleza shughuli ambazo zitawawezesha kuinua hali zao za maisha. Nafasi za majukumu ya vijana katika jamii hutegemea sana jinsi jamii inavyotoa kipaumbele kwa masuala ya malezi na maendeleo yao tangu wakiwa watoto wadogo ili waweze kuimarika kwa tabia na maadili. Vijana kama wananchi wengine wenye uwezo wa kufanya kazi, wana haki na wanapaswa kushirikishwa katika shughuli mabalimbali zenye lengo la kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

2.2 Suala la mchango wa vijana katika kuleta maendeleo ni jambo ambalo taifa linatakiwa kulitilia mkazo ili kuendeleza uwezo wao wa kujitegemea pamoja na kuwawezesha:-

2.2.1 Kutambua matatizo yao na matatizo ya taifa.

2.2.2 Kutambua uwezo na wajibu wao katika kuchangia maendeleo ya taifa.

2.2.3 Kubainisha, kuainisha na kutumia rasilimali zilizopo katika mazingira yao.

2.2.4 Kuamua, kupanga na kutekeleza mipango yao ya maendeleo ya jamii, kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa.

Ni kutokana na msingi huu Serikali imeona kuna umuhimu wa kuwa na sera ambayo itakuwa dira na kutoa mwongozo wa shughuli zote za maendeleo ya vijana.

## SURA YA TATU

## 3.0 MADHUMUNI YA SERA YA MAENDELEO YA VIJANA

3.1 Kuboresha maisha ya vijana, wake kwa waume kwa kuwaendeleza katika nyanja za uchumi, utamaduni, siasa, malezi,elimu na afya.

3.2 Kuhamasisha vijana na jamii katika kutambua, kukuza (promote) na kulinda haki za vijana kulingana na katiba ya nchi.

3.3 Kushirikisha idara, taasisi na vyombo mbalimbali katika kutekeleza mipango ya kuwaendeleza vijana kwa lengo la kudhibiti athari mbaya zinazotokana na michakato ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni.

3.4 Kuwaandaa vijana kimwili, kiakili, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni ili waweze kuchukua majukumu mbalimbali kama raia wema, wazazi na viongozi katika jamii.

3.5 Kuwawezesha vijana kushiriki katika juhudi za kuleta maendeleo ya jamii na taifa.

## SURA YA NNE

## 4.0 MALENGO NA MIPANGO YA MAENDELEO YA VIJANA

Ili kufanikisha utekelezaji wa sera ya maendeleo ya vijana, mipango ya maendeleo itakuwa na malengo yafuatayo.

### 4.1 Malengo

4.1.1 Kusambaza sera na kuhamasisha umma, taasisi na idara mbalimbali kuweza kuielewa na kuitekeleza.

4.1.2 Kulinda haki za vijana kama vile kupata elimu, kuajiriwa na kujiajiri, afya na kupata huduma, kupata malezi, lishe bora, burudani n.k.

4.1.3 Kubainisha mahali vijana walipo, idadi yao, shughuli zao na mahitaji yao ili kuweza kutumia takwimu hizo katika upangaji wa shughuli za maendeleo yao.

4.1.4 Kuwa na mipango mizuri ya ajira ambayo itawasaidia vijana kutatua matatizo yao ya ukosefu wa ajira na kuwawezesha kujitegemea kiuchumi.

4.1.5 Kuwa na mipango mizuri ya kutoa elimu ya mafunzo ya stadi ili kuwasaidia kuanzisha miradi yenye faida na kuiendesha ipasavyo.

4.1.6 Kuwahamasisha vijana, wake kwa waume kuanzisha na kuendesha miradi ya kiuchumi.

4.1.7 Kuwa na utaratibu mzuri wa kuwawezesha vijana kupata nyenzo za kazi, mitaji, maeneo ya kufanyia kazi na masoko ya bidhaa zao.

4.1.8 Kuwa na mtandao wa kupeana na kubadilishana habari kuhusu shughuli za maendeleo ya vijana.

4.1.9 Kuwa na mipango mizuri ya kuwaandaa na kuwashirikisha vijana, wake kwa waume katika shughuli za maendeleo ya kitaifa.

4.1.10 Kuwa na mipango mizuri ya malezi bora kwa vijana ili wawe wazazi bora na raia wema.

4.1.11 Kuwa na mipango mizuri ya kutoa huduma maalum za afya kwa vijana.

4.1.12 Kuboresha mazingira ya elimu na kuongeza nafasi za masomo katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo.

4.1.13 Kuwa na mipango ya kuwaendeleza kielimu wasichana wanaokatishwa masomo yao kutokana na kupata mimba.

## 4.2 Mipango

Kutokana na malengo yaliyotajwa hapo juu, mipango ifuatayo imeandaliwa ili kufanikisha maendeleo ya vijana.

4.2.1 Mipango ya kuhamasisha umma, taasisi, idara mbalimbali, vyama vya hiari, wazazi n.k. kuhusu sera ya maendeleo ya vijana.

4.2.2 Mipango ya utafiti na ukusanyaji takwimu za vijana na shughuli zao na kuanzisha mfumo wa kubadilishana taarifa zao.

4.2.3 Kupanua na kuimarisha soko la ajira hasa katika sekta isiyo rasmi.

4.2.4 Mipango ya mafunzo ya stadi na ujuzi mbalimbali.

4.2.5 Mipango ya kulinda haki za vijana.

4.2.6 Mipango ya elimu ya malezi.

4.2.7 Mipango ya afya kwa vijana.

4.2.8 Mipango ya kushirikisha vijana, wake kwa waume katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na kuwawezesha kuwa viongozi.

4.2.9 Mipango ya burudani.

4.2.10 Mipango ya ujasiri.

## SURA YA TANO

## 5.0 MAJUKUMU YA SEKTA MBALIMBALI KATIKA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO YA VIJANA

Shughuli za maendeleo ya vijana zinagusa karibu sekta zote za maendeleo. Hivyo katika kufanikisha shughuli hizi ni wajibu wa sekta zote zinazohusika kujumuisha masuala ya

maendeleo ya vijana katika sera, programu na miradi yao, pamoja na kushiriki katika utekelezaji wa programu mbalimbali za maendeleo ya vijana.

Sekta zinazogusa zaidi maendeleo ya vijana ni pamoja na sekta ya Ardhi, Afya, Elimu, Kilimo na Mifugo, Biashara na Viwanda, Maliasili na Utalii, Fedha, Mawasiliano, huduma za jamii, Madini, Tume ya Mipango, Serikali za Mitaa, Mashirika yasiyo ya Serikali, Mashirika na Makampuni ya watu binafsi. Jamii na familia wanalo jukumu la kutekeleza mipango ya masuala ya maendeleo ya vijana.

Wizara inayoshughulikia masuala ya maendeleo ya vijana ndiyo mratibu na msimamizi mkuu wa shughuli za Maendeleo ya Vijana nchini. Aidha Wizara hii ina jukumu la kuandaa sera na miongozo mbali mbali ya utekelezaji wa sera hiyo.

## 5.1 Familia

5.1.1 Zihakikishe vijana, wake kwa waume wanapata lishe bora.

5.1.2 Ziwahakikishie vijana haki kama vile upendo, usalama, ulinzi, maendeleo pamoja na kuwapa maadili mema na mahitaji mbalimbali.

5.1.3 Zihakikishe vijana wanakuwa na afya njema na kuwapatia elimu bila ubaguzi wa kijinsia.

5.1.4 Zihakikishe kuwepo na mshikamano wa kifamilia kwa kuwashirikisha vijana katika maamuzi.

## 5.2 Serikali za Vijiji

Serikali za vijiji zihakikishe:-

5.2.1 Vijana wanapata huduma muhimu za jamii.

5.2.2 Vijana wanapata misaada ya kuanzisha miradi yao ya kujiajiri na kujitegemea.

5.2.3 Kuwepo na mshikamano katika kuwarithisha vijana tabia njema, mila na desturi ili wakue wakifuata maadili mema.

5.2.4 Zinandaa mipango itakayoweza kutoa ajira kwa vijana katika maeneo yao.

5.2.5 Kuwa haki za vijana katika vijiji na mitaa zinalindwa.

## 5.3 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo Mijini

5.3.1 Iandae mipango na utaratibu utakaowawezesha vijana kupata ardhi na nyumba bila ku liwa.

5.3.2 Iweke utaratibu wa kujenga nyumba za kupanga kwa bei nafuu kwa ajili ya vijana ikiwa na lengo la kupunguza tatizo la makazi mijini.

5.3.3 Ipime na kutenga maeneo maalum kwa ajili ya vijana kuendesha shughuli zao za maendeleo na burudani.

## 5.4 Wizara ya Afya

5.4.1 Iwashirikishe vijana katika kuandaa, kupanga na kutekeleza programu za afya zinazolenga kuwaendeleza.

5.4.2 Ihakikishe upatikanaji wa huduma za afya ambazo vijana watazitumia bila woga, kunyanyaswa au kubaguliwa kwa aina yoyote hasa wa kijinsia.

5.4.3 Ihamasishe vijana na jamii katika kubaini matatizo ya kiafya yanayoathiri hususani magonjwa ya zinaa (STD), Ukimwi na utumiaji wa madawa ya kulenya.

5.4.4 Iandae programu maalum za kupambana na magonjwa ya zinaa, ukimwi, na utumiaji wa madawa ya kulevya.

5.4.5 Iimarishe programu za uzazi wa mpango kwa vijana bila kujali jinsia.

5.4.6 Iandae mitaala kuhusu afya ya vijana itakayotumika kufundishia wataalamu na wafanyakazi katika ngazi zote za sekta ya afya.

## 5.5 Wizara ya Biashara na Viwanda

5.5.1 Iandae programu itakayowawezesha vijana kubuni na kuendeleza miradi ya biashara na viwanda.

5.5.2 Iandae huduma za biashara na viwanda kama vile mafunzo, masoko, habari na teknolojia mbalimbali.

## 5.6 Wizara ya Elimu

5.6.1 Iimarishe na kueneza katika ngazi zote za elimu programu ya Elimu ya Familia.

5.6.2 Iendelee kuainisha mitaala mara kwa mara kulingana na mabadiliko ya wakati na mahitaji ya vijana.

5.6.3 Iimarishe Elimu ya Msingi kwa wote (UPE) na ipanuliwe hadi sekondari kidato cha nne.

5.6.4 Iimarishe masomo na mafunzo ya sayansi na teknolojia kwa kuzingatia vitendo zaidi.

5.6.5 Iendelee kuangalia na kutatua matatizo yanayosababisha wasichana kutojiunga na masomo au mafunzo ya sayansi na ufundi kwa lengo la kuandaa mikakati ya kuongeza idadi ya wasichana katika masomo hayo.

5.6.6 Iandae programu za kuwashirikisha vijana, wake kwa waume katika malezi yenye maadili mazuri ya utamaduni wa Watanzania.

## 5.7 Wizara ya Fedha

5.7.1 Itambue umuhimu wa vijana katika maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi katika taifa na itenge fedha zitakazotosheleza kuendesha programu zao.

5.7.2 Taasisi nyingine za fedha ziandae utaratibu wa mikopo yenye masharti nafuu ili kuwawezesha vijana kuanzisha na kuendesha miradi yao ya maendeleo.

## 5.8 Wizara ya Kilimo

5.8.1 Iandae programu za kilimo na ufugaji zinazowalenga vijana.

5.8.2 Iandae mikakati ya kutoa mafunzo ya kilimo na ufugaji bora kwa vijana kwa kutumia teknolojia sahihi ili kuongeza uzalishaji.

5.8.3 Ishirikiane na jamii katika kuwashirikisha vijana kuandaa taratibu za kuendesha mashindano ya kilimo na ufugaji bora.

## 5.9 Wizara ya Mendeleo ya Jamii

5.9.1 Ishirikiane kwa karibu zaidi na Wizara inayoshughulikia maendeleo ya vijana katika kuandaa mikakati maalumu ya pamoja ya kumwendeleza kijana wa kike.

5.9.2 Ihamasishe jamii kuhusu matatizo yanayoathiri maendeleo ya vijana wa kike na kuyatafutia ufumbuzi.

5.9.3 Iraghibishe utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana katika ngazi za kata hadi vijiji.

**5.10 Maliasili na Utalii**

5.10.1 Iandae programu za Maliasili na Utalii zinazowalenga vijana kuhusu uzalishaji mali kama vile uvuvi, nyuki, misitu, utalii n.k.

5.10.2 Iandae utaratibu wa kuwashirikisha vijana katika mipango ya hifadhi ya maliasili na mazingira.

**5.11 Wizara ya Madini na Nishati**

Iandae programu zinazowashirikisha vijana katika shughuli za uchimbaji wa madini, utoaji wa mafunzo, nyenzo na habari pamoja na kuweka mfumo mzuri wa masoko.

**5.12 Wizara ya Habari na Utangazaji**

5.12.1 Iandae programu za kuelimisha jamii na kuhamasisha utekelezaji wa programu za maendeleo ya vijana.

5.12.2 Iweke utaratibu ambao utaviwezesha vyombo vya habari kushiriki katika kuimarisha maadili mema ya vijana.

**5.13 Wizara ya Sheria na Katiba**

5.13.1 Iandae utaratibu utakaohakikisha uzingatiaji wa haki za vijana unatendeka kulingana na katiba ya nchi.

5.13.2 Iandae utaratibu wa kuwaelimisha vijana kuhusu haki zao za kikatiba.

## 5.14 Tume ya Mipango

5.14.1 Itaingiza programu za kutekeleza sera hii katika mipango ya maendeleo ya Taifa na kuhakikisha kuwa zinatekelezwa.

5.14.2 Itatambua umuhimu wa sera ya maendeleo ya vijana kama sehemu ya utekelezaji wa Sera ya idadi ya watu.

5.14.3 Itaviongoza na kuvielekeza vyombo vinavyohusika na upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika Sekta mbalimbali kuyapa masuala ya maendeleo ya vijana umuhimu unaostahili.

## 5.15 Serikali za Mitaa

Zihakikishe kuwa zinaingiza na kutekeleza programu za maendeleo ya vijana katika mipango yao.

## 5.16 Mashirika yasiyo ya Serikali na Makampuni Binafsi

Waandae mipango na taratibu za utekelezaji wa Sera ya maendeleo ya vijana.

## 5.17 Baraza na Kamati za Maendeleo ya Vijana

Pamoja na kuzishirikisha Sekta mbalimbali, vilevile kuna haja ya kuunda Baraza la Maendeleo ya Vijana na Kamati za Maendeleo ya Vijana ambazo zitasaidia kutoa ushauri katika kupanga na kutekeleza shughuli za vijana.

### 5.17.1 Wajibu wa Baraza la Maendeleo ya Vijana

Baraza la maendeleo ya vijana litaundwa na vikundi na mashirika ya vijana yaliyosajiliwa kuanzia ngazi ya wilaya hadi taifa. Wajibu wa baraza ni kama ifuatavyo:-

5.17.1.1 Kuwahamasisha vijana waweze kushiriki kikamilifu katika kutatua matatizo yao.

5.17.1.2 Kuunganisha vyama na vikundi mbalimbali vya vijana vinavyojiunga au vilivyojiunga kwa madhumuni maalum ya kimaendeleo na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria bila kujali jinsia, itikadi ya siasa, kabila au dini.

5.17.1.3 Kufanya utafiti na kukusanya takwimu mbalimbali zinazohusu vijana na shughuli za maendeleo yao.

5.17.1.4 Kuainisha na kuchambua matatizo na mahitaji ya vijana nchini kwa lengo la kuandaa mikakati ya kuyatafutia ufumbuzi.

5.17.1.5 Kubuni mipango na kuandaa programu na miradi katika sekta mbalimbali kwa lengo la kutatua matatizo ya vijana na kuwashirikisha katika shughuli za maendeleo ya taifa.

5.17.1.6 Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa mipango yote ya maendeleo ya vijana nchini, hii ikiwa ni pamoja na zile zinazotekelezwa na vyama vya hiari na mashirika.

5.17.1.7 Kutekeleza sera mbalimbali zinazoandaliwa na taifa kama vile kampeni za mazingira, usafi n.k. kama mchango wao katika maendeleo ya Taifa.

5.17.1.8 Kuwaunganisha vijana wa Kitanzania na vijana wa mataifa mengine kushirikiana katika masuala yanayohusu maendeleo yao na mataifa yao.

5.17.1.9 Baraza litahusika na usajili wa vyama au vikundi vyote vya vijana. Litakuwa chombo cha kuishauri Serikali kuhusu masuala yanayohusu haki na maslahi kwa ajili ya maendeleo ya vijana.

## 5.18 Muundo wa Baraza

Baraza la maendeleo ya vijana litaundwa na vyama au vikundi vya vijana kuanzia ngazi ya wilaya hadi taifa vilivyosajiliwa kwa madhumuni maalumu ya kutatua matatizo yanayowakabili vijana.

## 5.19 Wajibu wa Kamati za Maendeleo ya Vijana

5.19.1 Kutoa ushauri kwa Serikali na vijana wenyewe juu ya utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo ya vijana.

5.19.2 Kusaidia kuanzisha na kuimarisha mfuko wa fedha wa masharti nafuu katika maeneo yao ili vijana waweze kufaidika kwa kukopa fedha.

5.19.3 Kuwa wadhamini wa vikundi vya vijana vya uzalishaji mali ili kuvisaidia kupata misaada

mbalimbali kutoka mashirika, wahisani, mabenki n.k.

5.19.4 Kusaidia programu za vijana katika maendeleo mbalimbali yatakayojitokeza.

## 5.20 Muundo wa Kamati

Kamati hizi zitaundwa na wajumbe kutoka vikundi vya vijana vya uzalishaji mali (VVKM), vyama vya hiari vinavyoshughulikia maendeleo ya vijana, wajumbe wa kàmati za maendeleo za vijiji, Kata, Wilaya na Mikoa, madiwani na watu binafsi wanaokereketwa na masuala ya vijana. Wajumbe kutoka sekta (Idara) za Serikali, Mabenki na mashirika ya umma wataalikwa kuhudhuria vikao kama wataalamu na kazi yao kubwa itakuwa kutoa ushauri (angalia kiambatanisho No. 1).

## TAMATI

Wizara inayoshughulikia maendeleo ya vijana kwa kushiri
sekta zinazohusika zitakuwa zinaandaa utaratibu wa kufan)
na tathmini kila inapohitajika ili kuboresha utekelezaji wa s(

Kiambatisho No. 1

## KAMATI YA MKOA YA MAENDELEO YA VIJANA

Kamati ya Mkoa ya Maendeleo ya Vijana itakuwa na wajumbe wafuatao:-

1. Mkuu wa Mkoa - Mwenyekiti
2. Waheshimiwa Wabunge kutoka kila Wilaya
3. Diwani mmoja kutoka kila Wilaya
4. Wawakilishi wawili kutoka kila Wilaya wanaowakilisha VVKM
5. Mwenyekiti wa Shule za Sekondari za Mkoa
6. Mwakilishi mmoja kutoka Vyama vya hiari, Umma na Mashirika ya dini
7. Katibu Tawala wa Mkoa
8. Wakurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya
9. Mwananchi mmoja mkereketwa wa shughuli za vijana
10. Afisa Maendeleo ya Vijana - Katibu
11. Wataalam kutoka sekta mbali mbali kama waalikwa

## KAMATI YA WILAYA

Kamati ya Wilaya itakuwa na wajumbe wafuatao:-

1. Mkuu wa Wilaya - Mwenyekiti
2. Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya
3. Mheshimiwa Mbunge
4. Mwakilishi mmoja kutoka shule za sekondari
5. Madiwani (3)
6. Mwakilishi mmoja kutoka, vyuo
7. Mwakilishi mmoja wa VVKM kutoka kila kata

8. Mwakilishi mmoja kutoka vyama vya hiari/mashirika ya dini kutoka Wilaya
9. Wananchi wawili wakereketwa wa shughuli za vijana (Mwanamke na Mwanaume)
10. Afisa Maendeleo ya Vijana - Katibu
11. Wataalam waalikwa kama wajumbe

## KAMATI YA KATA

Kamati ya Kata itakuwa na wajumbe wafuatao:-

1. Diwani - Mwenyekiti
2. Mratibu wa Elimu
3. Katibu mmoja kutoka Kata
4. Mjumbe mmoja kutoka kila kikundi cha VVKM
5. Mwakilishi mmoja kutoka vyama vya hiari na mashirika ya dini
6. Mwananchi mmoja mkereketwa wa shughuli za vijana
7. Katibu Kata - Katibu
8. Wataalamu waalikwa kama wajumbe.

## KAMATI YA KIJIJI YA MAENDELEO YA VIJANA

Kamati ya Kijiji ya Maendeleo ya Vijana itakuwa na wajumbe wafuatao:-

1. Mwenyekiti wa Kijiji - Mwenyekiti
2. Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi
3. Mwakilishi (Vyama vya Hiari)
4. Wawakilishi 2 kutoka VVKM
5. Wananchi wawili wakereketwa wa shughuli za vijana (Mwanamke na Mwanaume)

6. Katibu wa Kijiji - **Katibu**
7. Wataalam wataalikwa.

## IDADI YA VIJANA WALIOCHAGULIWA NA AMBAO HAWAKUCHAGULIWA KUINGIA KIDATO CHA I KIPINDI CHA 1980 - 1991

| MWAKA | WALIO CHAGULIWA | WALIO CHAGULIWA NA KUINGIA KIDATO CHA '1' SERIKALINI/ BINAFSI | % | AMBAO HAWAKUCHA GULIWA | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1980 | 212,446 | 16,098 | 7.5 | 196,438 | 92.5 |
| 1981 | 657,816 | 17,166 | 4.8 | 340,050 | 95.2 |
| 1982 | 410,829 | 17,710 | 4.2 | 402,119 | 95.8 |
| 1983 | 454,604 | 19,605 | 4.3 | 435,099 | 95.7 |
| 1984 | 649,560 | 21,322 | 3.4 | 627,738 | 96.6 |
| 1985 | 420,192 | 23,506 | 6.5 | 405,688 | 94.5 |
| 1986 | 380,096 | 27,430 | 7.2 | 352,666 | 92.8 |
| 1987 | 380,758 | 32,633 | 8.6 | 348,125 | 91.4 |
| 1988 | 347,978 | 56,464 | 10.6 | 311,514 | 89.5 |
| 1989 | 267,744 | 42,136 | 15.7 | 225,608 | 84.3 |
| 1990 | 306,656 | 47,227 | 15.4 | 259,429 | 84.6 |
| 1991 | 383,427 | 19,282 | 5.1 | 364,145 | 94.9 |

Chanzo: Basic Education Statistics for Tanzania 1991